Imani ya Kweli

na

Ellis P. Forsman

Imani ya Kweli

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Imani ya Kweli

1 Petr. 1:7

1 Petr. 1:7, "*Ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo inathamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa wenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Kristo Yesu.*"

Imani ya kweli ni imani kamilifu. Haipatikani kwenye boksi, kama viazi vya kufikia. Inajengwa kama viazi vinavyo kuwa katika shamba. Inachukua muda na juhudi. Zawadi zake ni za ajabu.

Katika fungu letu la maandiko Paulo anawasifu Wakristo wasomaji wake kwa imani yao ya kweli. Imani yao ilikuwa ya kweli na haikutikisika hata katika mateso.

Imani ya kweli ni imani ianayoongozwa na kweli. Ni yenye nguvu na uwezo. Kwavile imeagizwa na Roho Mtakatifu, Wakristo wanapaswa kutamani kuwa nayo. Pasipo hiyo hatuna tumaini. Imani ya kweli ni lazima kuwa nayo.

Hebu tuangalie ni nini tunaweza kujifunza kuhusu imani ya kweli.

Imani ya kweli inakuwa juu ya kweli

Imani ya kweli huja kwa kuisikia kweli.

Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Neno la Mungu ni kweli. Yoh. 17:17, "*Unitakase na neno lako; neno lako ndio kweli.*"

Imani inaweza kuwa ya uongo kama hako juu ya kweli. Mfano: Shetani na Hawa.

Ni kweli pekee ndio hutuweka huru. Yoh. 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"

Imani inatakasa roho. 1 Petr. 1:22, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hatakuufikia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.*"

Roho zetu haziwi safi kama tukiujaza na kila aina ya uchafu, ya kidunia, au kidini.

Imani ya kweli huja kwa kweka bidii katika kusoma.

Kama tuna imani ya kweli tumechukua muda wa kuipata. Tumechukua muda na tumejizungushia sisi wenyewe na vifaa vya msaada vinavyotusaidia kupata ujuzi wa maandiko (Biblia, konkodensi, nk).

Kujifunza kwetu lazima iwe kila siku, kama ilivyokuwa kwa Waberoya.

Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Imani dhaifu haiwezi kuwa imani ya kweli. Hawa ndugu waliitaji kweli – ilikuwa ya kweli.

Imani ya kweli uishi kwayo

Tukijijaza sisi wenyewe na neno la Mungu lazima ijionyeshe yenyewe.

Yer. 20:9, "*Nami nikisema sitamtaja wala sitasema kwa jina lake; basi ndipo moyoni mwangu kumekuwamo kama moto uwakao, uliofungwa ndani ya mifupa yangu, nami nimechoka kwa kustahimili, wala siwezi kujizuia.*"

Wakristo wachanga wako hivyo wanapojifunza kweli na kuungana na Bwana katika ubatizo. Wanajawa na moto kwa ajili ya Bwana.

Ujuzi unaleta upendo wa Mungu.

1 Yoh. 4:19, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"

Upendo unajionyesha wenyewe kwa kumtumikia yule aliyependwa.

- Yoh. 14:15, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"
- 1 Yoh. 2:5, "*Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.*"

Pasipo ujuzi wa neno la Mungu, hatuwezi kujua kwamba "*tumo ndani yake.*"

Imani ya kweli inatenda kazi katika huduma.

Tukiwa na imani ya kweli kunakuwa na dalili ya mabadiliko kwa namna tunavyoishi.

Rum. 8:5-6, "*Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waufuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani.*"

Mtu anapokuwa na imani ya kweli inapoona ukweli atahitaji kubadilisha maisha yake na kuishi kwa ukweli. Kuna madiliko yanayoonekana katika tabia ya mtu.

Kol. 3:1-5, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofufuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Maana vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu;*"

Kufisha – uwa, haiwezi kuishi au kutenda kazi, weka pembeni.

Wakati ukweli wa neno la Mungu unapotuambia kwamba tunapaswa kubadilika unasaidia moyo. 2 Tim. 2:22, "*Lakini zikimbie tamaa za ujanani, ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi.*"

Mabadiliko yataonekana kiasi kwamba marafiki zako wa kidunia watadhani kwamba wewe ni mgeni. 1 Petr. 4:4, "*Mambo ambayo wao huona kuwa ni ajabu ya ninyi kuto kwenda mbio pamoja nao katika ufisadi ule ule usio na kiasi, wakiwatukana.*"

Tunapokuwa na imani ya kweli baada ya kujifunza neno la Mungu, ndipo tutatamani kuishi katika tunda la Roho. Gal. 5:22-23, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utuwema, fadhili, uaminifu, upole kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*"

Hii ndio aina ya maisha ambayo imani ya kweli itatuongoza. Kwa sababu ya imani ya kweli, mtu atahitaji kufanya mema kama Bwana pia alivyofanya.

Mdo. 10:38, "*Habari za Yesu wa Nazareti jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka zunguka huku na huko akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi, kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.*"

Hata kama hatukukirimiwa uwezo ambao Yesu alikuwa nao, kuna mengi ambayo tunaweza kufanya, hataivyo. Kujitoa kwetu ni kwa Mungu; kumsifu kwa kutenda katika kweli yake. 1 Kor. 6:20, "*Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuseni Mungu katika miili yenu.*"

Imani ya kweli inanguvu (haitetereki)

Imani ya kweli haitetereki wakti wa matatizo na shida. Wakristo wa kwanza waliishi kwa uaminifu walipokuwa wakikumbana na mateso.

Imani ya kweli unamtazama Mungu na ahadi zake zaidi ya matatizo ya kidunia ambayo tunapaswa kuyavumilia. Paulo aliandika kuhusiana na vitu alivyovumilia kwa sababu ya Kristo.

Rum. 8:18, "*Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.*"

Imani kama hiyo utasimama katika jaribu lo lote.

Kwa macho ya kuona, tunapaswa kujaribu kuwa na imani yenye nguvu kupitia kujifunza na kuomba. Kama imani yetu ikifa, tumaini letu na upendo utakufa pamoja nayo.

Marko 4:16-17, "*Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye mwamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache, kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa.*

Imani ya kweli una moyo wa upendo

Imani ya kweli hutenda kazi ya Mungu kwa nia njema. Yote tunayoyafanya lazima yafanyike kwa roho ya upendo.

1 Kor. 13:1-3, "*Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii na kujua siri zote na maarifa yote; nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo hainifaidii kitu.*"

Mtu anaweza kuwa na imani ya Mungu, lakini kama hana upendo kwa ajili ya wengine anapowapa ukweli, watageuka kutoka katika kweli. Paulo alisema kwamba imani hutenda kazi <u>kupitia</u> upendo.

Gal. 5:6, "*Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, <u>bali imani itendayo kazi kwa upendo.</u>*"

Imani ya kweli sio tu kwamba inafanya kile ambacho Mungu anahitaji, lakini pia kwa nia njema.

Hitimisho

Tumeshaona mambo muhimu ya imani ya kweli. Imani inayoagizwa na Roho Mtakatifu. Ni mfano wa Wakristo kufuata.

Mkristo wa kweli anapaswa kusema, "Nina hitaji imani hii." Ni imani itakayozaa mambo makuu katika huduma ya Mungu na Kristo. Zawadi iliyoko wakati wa mwisho wa maisha haya ni kuu.

Wakristo: Pasipo imani hii ya kweli hatutampendeza Bwana ama kushinda majaribu ya maisha. Lazima tupende kuweka muda na nguvu

lakini inahitajika kuwa na imani hii ya kweli. Tunapswa tutubu kama tunalikataa hili.

Ambao hawajaokolewa: Mnapaswa kujibu mwaliko wa Bwana na kufanyika Wakristo.

Hii itakuanzisha katika safari yako ya kiroho katika kuhitaji imani ya kweli ambayo itakuweka imara kupitia maisha haya.

Je wewe ni Mkristo? Au unakaribia kufanyika Mkristo?

Mtu anafanyikaje Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; maana kila amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wote wamtafutao.*" Nilipokuwa katika shule ya sekondari (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja rika moja na mimi akaniambia kwamba hakuamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kama kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu yenye usalama, labda aende kanisani, na siku akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mema Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nika mwambia "haiendi hivyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote pasipo hivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba nyingine, na ukafikiria mwenyewe kwamba "kuna mwizi ndani ya nyumba yangu!" alafu unachukua simu ya mkononi, kwa taratibu unawaita polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani ya nyumba yako, unawapa anwani ya nyumba yako. Kidoho unasikia wanafika na kumkamata mwizi. Alafu anapiga kelele, "Samahani, samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwamba amekamatwa. Katika toba ya kweli mwizi alipaswa kuomba msamaha kwamba hataiba na kwamba anataka kubadili maisha yake na kwamba hataiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la akili linaloleteleza badiliko la tendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kukiri**. Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (Kuamini), kutubu, na kukiri ni **KATIKA** haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kitu fulani; sio kwamba mtu tayari amepata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ni nayependezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kufanya. Unaona ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "*Imekuwa **kwetu sisi** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, sio kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, kama hatujabatizwa bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe huku ukiliitia jina la Bwana.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu*

kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." (War. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (War. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu ya kutumia kwa damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapo batizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?